

*Swahili*



*53 Prospect Road, Gaythorne, Q 4051*

*simu 07 3354 4900*

*baruapepe info@amparo.org.au*

**Tunasimama kwa ajili ya...**

**watu kutoka asili tofauti za kitamaduni na kilugha wenye ulemavu**

wanaotendewa bila haki, kunyanyaswa au kubaguliwa.

Tunafanya kazi nawe kulinda haki zako za kibinadamu na kuhakikisha  
mahitaji yako ya kimsingi yanatimizwa.

*simu (07) 3354 4900*

# sisi ni nani...

## AMPARO Advocacy Inc

ni shirika lisilo la faida la jamii  
linalofadhiliwa na Serikali ya  
Queensland ili kutoa Utetesi  
wa kujitegemea.

**Tunatetea kwa ajili ya watoto  
na watu wazima wenye umri  
chini ya miaka 65.**

# tunaamini

## Watu kutoka asili tofauti za kitamaduni na kilugha wenye ulemavu wana haki ya:

- kuheshimiwa na kuthaminiwa
- kuunganishwa na jamaa na marafiki
- kupata wakalimani na taarifa zilizotafsiriwa
- kutolewa misaada na huduma kwa njia za mwitikio wa kitamaduni
- kujumuishwa katika jamii
- kuwa na fursa ya kuishi maisha mazuri

# tunachofanya...

## AMPARO Advocacy:

- itakufahamu na kuelewa hali yako
- itazingatia mahitaji yako muhimu zaidi
- itabainisha njia zinazofaa kitamaduni za kufanya kazi nawe
- Itakupa maelezo kuhusu haki zako na huduma ambazo zinaweza kukusaidia
- Itakuunga mkono kuelewa taarifa, kufanya maamuzi na kuzungumza wasiwasi
- Daima itakuwa upande wako